AFISI YA RAIS, KAZI, UCHUMI NA UWEKEZAJI

# JARIDA LA UCHUMI NA UWEKEZAJI

ISNN 1290-2018 TOLEO NA. 001 APRIL - SEPTEMBA 2023

**TUJIAJIRI KWA KUKUZA UCHUMI NA KULETA MAENDELEO ZANZIBAR**



## UWEKEZAJI NI SEKTA MUHIMU KWA MAENDELEO YA NCHI KATIKA KUKUZA UCHUMI NA KUZALISHA AJIRA

# BODI YA WAHARIRI


**WASHAURI**

Bi Maryam Juma Abdulla

Dkt. Habiba Hassan Omar

**MHARIRI**

Bahati Ahmad Abdalla

**WASANIFU PICHA**

Saadam Seif Ali

Samiya Ali Haji

**MTAALAMU TEHAMA**

Ubwa Amuni Ubwa

**MUONGOZAJI**

Bahati Ramadhan Ali



Imetolewa na Kitengo cha
Habari na Uhusiano
Afisi ya Rais Kazi Uchumi na
Uwekezaji



Mtaa wa Kificho - M/Kwerekwe
S.L.P 884 Zanzibar
Simu Na 0242230061
Fax: 0242230062

Email: info@arkuusmz.go.tz

Tovuti: www.arkuusmz.go.tz


# YALIYOMO


| | |
|---|---|
| Uongozi wa ARKUU | 01 |
| Salamu za Mheshimiwa Waziri | 02 |
| Dira, Dhamira na Muundo | 03 - 04 |
| Mafanikio na Mikakati ya Afisi. | 05 - 08 |
| ZIPA katika Kukuza Uwekezaji Nchini | 09 - 10 |
| Ujasiriamali ni Ajira | 11 - 12 |
| Utekelezaji wa Sheria za Kazi | 13 - 15 |
| Fursa za Ajira kwa Vijana. | 16 |
| Ifahamu OSH - Zanzibar. | 17 - 18 |
| Ushirikiano wa Sekta ya Umma na Sekta Binafsi katika Uwekezaji | 19 - 20 |
| Matukio katika Picha | 21 - 23 |
| Wasemavyo | 24 |
| Wadau wetu | 24 |

# UONGOZI WA AFISI YA RAIS, KAZI, UCHUMI NA UWEKEZAJI



**MHE. MUDRIK RAMADHAN SORAGA**
**Waziri wa Nchi Afisi ya Rais, Kazi, Uchumi na Uwekezaji**



**BI. MARYAM JUMA ABDULLA**
**Katibu Mkuu (Kazi na Uwezeshaji)**
**Afisi ya Rais, Kazi Uchumi na Uwekezaji**



**DKT. HABIBA HASSAN OMAR**
**Katibu Mkuu (Uchumi na Uwekezaji)**
**Afisi ya Rais, Kazi Uchumi na Uwekezaji**



**BI. HALIMA MAULID SALUM**
**Naibu Katibu Mkuu (Kazi na Uwezeshaji)**
**Afisi ya Rais, Kazi Uchumi na Uwekezaji**



**NDG. KHATIB MWADINI KHATIB**
**Naibu Katibu Mkuu (Uchumi na Uwekezaji)**
**Afisi ya Rais, Kazi Uchumi na Uwekezaji**

# SALAMU ZA MHE. WAZIRI



**MHE. MUDRIK RAMADHAN SORAGA**
**Waziri wa Nchi Afisi ya Rais, Kazi, Uchumi na Uwekezaji**

Jarida la Uchumi na Uwekezaji linalotolewa na Afisi ya Rais, Kazi, Uchumi na Uwekezaji lenye lengo la kuelimisha jamii juu ya shughuli zinazotekelezwa na Afisi ikiwemo mafanikio, changamoto, mikakati na fursa zilizopo katika Afisi ya Rais, Kazi, Uchumi na Uwekezaji kwa kipindi cha miezi sita (06).

Nachukua fursa hii adhimu kukukaribisha msomaji wa Jarida hili la **Uchumi na Uwekezaji.**

Kwa kipindi cha miezi sita (06) kuanzia Aprili hadi Septemba 2023, Afisi imeshuhudia mafanikio makubwa ya kiutendaji ikiwemo mazingira mazuri ya kisera na kisheria katika kuwawezesha wananchi kiuchumi kwa kutoa mikopo, mafunzo pamoja na kuwaunganisha na fursa za masoko.

Aidha,Afisi inaendelea kuratibu upatikanaji wa ajira za staha ndani na nje ya nchi na kusimamia uzingatiaji wa Sheria na viwango vya kazi Kitaifa, Kikanda na Kimataifa .

Vile vile, Afisi imeimarisha mazingira ya kukuza na kusimamia uwekezaji nchini pamoja na kusimamia vyema miradi ya PPP.

Aidha, napenda kuishukuru Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar chini ya uongozi wa **Mhe. Dkt. Hussein Ali Mwinyi Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi** kwa kuwa karibu nasi kwa kutupa busara na miongozo mizuri katika kutekeleza majukumu yetu ya kila siku. Vile vile, napenda kuwashukuru wadau wote wakiwemo Wananchi, Wawekezaji, Mawakala Binafsi wa Ajira, Taasisi mbalimbali za Kifedha, Vyama vya Wafanyakazi, Jumuiya za Waajiri, Vyombo vya Habari pamoja na wadau wengine kwa kushirikiana nasi katika kuendeleza gurudumu la maendeleo.

# DIRA, DHAMIRA, MUUNDO



## AFISI YA RAIS, KAZI, UCHUMI NA UWEKEZAJI

## DIRA

Kuwa na Jamii ya Wazanzibari inayojiweza, iliyoendelea na kuimarika kiuchumi.

## DHAMIRA

Kuimarisha hali ya kijamii na kiuchumi ya wananchi wa Zanzibar kwa kutoa na kutumia fursa za kiuchumi zilizopo na zitakazokuja, kushajihisha utamaduni na uwezo wa ujasiriamali, kukuza uwekezaji wa ndani na nje, upatikanaji wa kazi za staha na kuzingatia sheria na viwango vya kazi.

## MUUNDO

Afisi ya Rais Kazi, Uchumi na Uwekezaji ina jumla ya watendaji 347-Unguja ni 274 (wanaume 122 na wanawake 152) na Pemba ni 73 (wanaume 41 na wanawake 32).

Afisi ya Rais Kazi, Uchumi na Uwekezaji ina Idara Saba (7), Afisi Kuu Pemba na Vitengo sita (6) vinavyoripoti moja kwa moja kwa Makatibu Wakuu. Aidha, Afisi ya Rais – Kazi Uchumi na Uwekezaji ina jumla ya Taasisi mbili (2) zinazojitegemea na Bodi nne (4). Mchanganuo wa Idara, Afisi Kuu, Taasisi, Bodi na vitengo ni kama ifuatavyo:-

INAENDELEA UK. 04

# IDARA

- Idara ya Ajira
- Idara ya Usalama na Afya Kazini
- Kamisheni ya Kazi
- Idara ya Maendeleo ya Vyama vya Ushirika
- Idara ya Mashirikiano baina ya Sekta ya Umma na Sekta Binafsi
- Idara ya Uendeshaji na Utumishi;
- Idara ya Mipango, Sera na Utafiti; na
- Afisi Kuu – Pemba.

# TAASISI

- Mamlaka ya Uwekezaji Vitega Uchumi Zanzibar (ZIPA)
- Wakala wa Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi (ZEEA)


# BODI

- Bodi ya Mishahara
- Bodi ya Ushauri wa Kazi
- Bodi ya Wakurugenzi Mamlaka ya Uwekezaji
- Bodi ya Wakala wa Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi

# MAJUKUMU

- Kuratibu uandaaji na Kusimamia utekelezaji wa Sera, Sheria, Miongozo na Mipango inayohusiana na Kazi, Ajira, Uwekezaji, PPP na Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi.
- Kukuza na kusimamia ufanisi wa utendaji wa kazi.
- Kuimarisha Programu za Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi
- Kuratibu upatikanaji wa mitaji na mikopo nafuu kwa Wajasiriamali na Wafanyabiashara nchini
- Kuimarisha upatikanaji wa mafunzo na masoko kwa bidhaa za Wajasiriamali na Wafanyabiashara
- Kuimarisha na kuratibu ufanyaji wa tafiti ili kuimarisha Mipango na Maamuzi ya kuendeleza jamii
- Kukuza, kuimarisha na kusimamia uwekezaji
- Kuimarisha Usalama na Afya Kazini.
- Kusimamia na kuratibu miundombinu ya Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi
- Kuandaa mikakati ya kuongeza fursa za ajira kwa kukuza ujuzi ndani na nje ya nchi pamoja na kazi za Staha kwa wote katika sekta binafsi
- Kusimamia, kukuza na kufanya mageuzi ya Sekta ya Ushirika
- Kusimamia utekelezaji wa Mikataba, Sheria na Kanuni za Kazi za Kitaifa, Kikanda na Kimataifa na kuimarisha mahusiano mazuri ya Kazi miongoni mwa Serikali, Sekta Binafsi, Waajiri na Vyama vya Wafanyakazi
- Kuhakikisha sekta ya umma na binafsi zinazingatia Sheria za ajira na Sheria za kazi.

# MAFANIKIO YA AFISI YA RAIS, KAZI, UCHUMI NA UWEKEZAJI (KAZI NA UWEZESHAJI)



**BI. MARIAM JUMA ABDULLA**

**Katibu Mkuu (Kazi na Uwezeshaji) Afisi ya Rais, Kazi Uchumi na Uwekezaji**

Kwa kipindi cha Aprili hadi Septemba 2023 Afisi imefanikiwa kufanya mambo kadhaa ambayo kwa kiasi kikubwa yameweza kuleta mabadiliko nchini. Mabadiliko hayo yamefanyika kupitia uongozi na watendaji wake wenye ari, weledi na utaalamu wa kutosha katika nyanja tofauti.

Kwa kuanzia katika masuala ya Kazi na Uwezeshaji. Afisi imefanikiwa kufanya ukaguzi katika Taasisi za Sekta binafsi 129 Unguja na Pemba (71 Unguja na 58 Pemba ) ikiwemo Sekta ya mahoteli, viwanda, kilimo pamoja na Sekta ya ujenzi ili kuweza kuhakikisha kuwa Sheria za Kazi zinatekelezwa. Vile vile, imeweza kutoa vibali vya kazi kwa wafanyakazi wa kigeni 1,265 ambapo waliopata msamaha wa Mhe. Waziri ni wafanyakazi 67, waliopata msamaha wa ZIPA ni wafanyakazi 70, Vibali vipya ni 346, Vibali vilivvo ongezwa muda ni 488 na vibali vya muda mfupi ni 276. Vibali vyote hivi ni kutoka katika Mataifa mbalimbali kama vile Zambia, Ujerumani, Yemeni, Amerika, Sudani na Kanada, ambapo vibali vyote hivyo vimeingiza jumla ya Tsh 725,914,927 kwa Serikali. Aidha, imeweza kuthibitisha Mikataba ya Kazi kwa wafanyakazi Wazawa 4,766 (4274 Unguja na 492 Pemba).

Pamoja na kupokea migogoro ya kazi 122 iliyowasilishwa katika Kitengo cha Usuluhishi na Uamuzi wa Migogoro ya Kazi, kati ya hiyo migogoro 18 imemalizika katika hatua ya usuluhishi, migogoro inayoendelea ni 48, migogoro inayoendelea katika hatua ya usuluhishi ni 49 na migogoro iliyomalizika ni 7.

Kwa kipindi cha miaka mitano 2023/2027 Afisi imejiwekea mkakati wa kuimarisha utekelezaji wa Sheria za Kazi, kupunguza tatizo la Ajira za watoto Zanzibar pamoja na kupunguza migogoro ya kazi nchini. Kufanya ukaguzi katika Wilaya zote za Unguja na Pemba kwa lengo la kuhakikisha Sheria za Kazi zinafatwa ipasavyo.

Aidha, Afisi imesimamia programu ya kujenga uzoefu wa kazi (Intership), ambapo Vijana 50 (wanaume 21 na wanawake 29) wamepata mafunzo hayo kwa ajili ya kuwaandaa na kuwajengea uwezo wa kujiamini wa kufanya kazi katika fani ya hotelia, ufundi gereji, ualimu na ushoni.

Pia, imefanikiwa kusajili jumla ya Taasisi mpya mbili za Mawakala Binafsi wa Ajira zilizotimiza vigezo ambazo ni Sashamark na Mahasna na kuzifanyia ukaguzi taasisi nne zinazokusudia kuongeza muda wa leseni ili ziweze kuendelea na shughuli zao. Taasisi hizo ni IBS Zanzibar Limited, Afnan Recruitment Agency, Blue Ageny Company Limited na Dejure Attorney. Hivyo, kwa sasa kuna jumla ya Taasisi za Uwakala Binafsi wa Ajira kumi na nne (14). Kutokana na usajili na ulipaji wa vibali vya wafanyakazi wanaokwenda kufanyakazi nje ya nchi afisi imeingiza jumla ya Tsh 41,415,000.

Kwa kushirikiana na Wakala Binafsi wa Ajira, Afisi imeratibu upatikanaji wa ajira za staha nje ya nchi kwa vijana 612 (Wanawake 493 na Wanaume 119), katika kazi za udereva, kazi za majumbani, vibarua wa ujenzi na kusambaza mizigo katika Nchi za Oman, Qatar, Saudi-Arabia na Visiwa vya Sheli sheli.

Afisi pia imepanga kutekeleza programu za kukuza ujuzi kwa vijana ili waweze kujiajiri na kuajirika kwa kuwajengea uelewa katika masuala ya Ajira na kuendelea kuwaunganisha vijana na fursa za Ajira za ndani na nje ya nchi. Aidha, kuwa na Mfumo imara wa Taarifa za soko la Ajira ambao utawawezesha vijana kujua fursa za ajira zilizopo katika sekta mbali mbali.

Mbali na hayo, Afisi imefanikiwa kufanya usajili wa sehemu za kazi 28 (Unguja 19 na Pemba 9) kwa ajili ya usalama na afya kazini na kuzitambua sehemu zilipo na shughuli zinazofanyika ili kuweza kufanya tathmini za hatari zinazoweza kutokea katika maeneo ya kazi. Usajili huo umeweza kuongeza pato la Tsh 58,890,600 kwa Serikali.

Pamoja na kufanikiwa kufanya ukaguzi katika Taasisi za Umma na Taasisi Binafsi 90 (Unguja 44 na Pemba 46) na kuwashauri waajiri kuweka mazingira bora ya kazi ili kuepusha matukio ya ajali na maradhi yatokanayo na kazi yasitokee kwa wafanyakazi na waajiri. Pia ilifanya uchunguzi wa ajali Saba (7) zinazotokana na kazi zilizoripotiwa na kutoa ushauri stahiki kwa wafanyakazi na waajiri kuhusiana na mazingira bora ya kazi ili kuepusha ajali kama hizo zisijirudie tena.

Aidha, Afisi kwa kipindi cha miaka mitano 2023/2027 imepanga kufanya ukaguzi katika Taasisi zaidi ya 1,500 pamoja na kufanya tathmini ya hatari na maradhi katika sehemu za kazi .Vile vile, kurekebisha Sheria na kuandaa Kanuni kwa ajili ya Afya na Usalama kazini ikiwemo Kanuni ya kutoa huduma ya kwanza na Kanuni ya kutoa ripoti kwa wakati.

Afisi pia imefanikiwa kusajili vyama vya Ushirika 579 (Unguja 278 na 301 Pemba) na kukagua hesabu za vyama 162(Unguja 152 na Pemba 10) pamoja na kutoa mafunzo juu ya dhana ya ushirika, usimamizi wa fedha , taratibu za usajili, ujasiriamali na utunzaji wa kumbukumbu kwa washiriki 1,703 (wanawake 992 na wanaume 711).Jumla ya Tsh 42,948,450 zimekusanywa na kuingia katika Serikali.

Afisi imejiwekea mikakati ya kufanya mageuzi ya sekta ya ushirika nchini kwa ajili ya kuvijengea uwezo vyama hivo kuwa imara na kuweza kusaidia kuleta maendeleo nchini.

Pia, kwa kipindi cha miezi sita Aprili hadi Septemba Afisi imefanikiwa kutoa mikopo yenye thamani ya Jumla ya Shilingi Bilioni Moja, Milioni Mia Sita Sitini Na Tisa, Laki Saba Na Elfu Kumi (TZS. 1,669,710,000) kupitia fedha za INUKA (Unguja TZS 907,210,000 na Pemba TZS 762,500,000), ambazo zimewanufaisha wananchi 620 (Unguja 188 na Pemba 432). Aidha, imeratibu utoaji wa mikopo kupitia Programu ya Mfuko wa Khalifa yenye thamani ya Jumla ya Shilingi Milioni Mia Moja Na Arubaini (TZS.140, 000,000) kwa viwanda viwili (2).

Pamoja na kufanikiwa kukagua na kutathmini maombi mapya 75 (Unguja 29 na Pemba 46) ya mikopo kupitia programu ya Inuka yenye thamani ya TZS 2,781,915,600. (Pemba TZS 799,932,000 na Unguja TZS 1,981,983,600). Kati ya maombi hayo, maombi 14 ni ya wawekezaji wa ndani (local investors) yenye thamani ya TZS 271,000,000.



*Mkurugenzi Mtendaji wa ZEEA Ndg Juma Burhan Mohamed akizungumza na wajasiriamali wa Zanzibar walioshiriki katika maeneosho ya 47 ya kimataifa ya saba saba jijini Dar es Salaam.*

Afisi imepanga kutoa mafunzo kwa wjasiriamali na wafanya biashara kuhusiana na mitaji na matumizi sahihi ya fedha; kuimarisha mashirikiano mazuri na Taasisi za Kifedha ili kutoa huduma nzuri kwa wafanyabiashara na wajasiriamali kwa kutoa na kusimamia upatikanaji wa mitaji yenye masharti nafuu katika kuwawezesha wajasiamali kupitia program za Khalifa Fund, Inuka na Mkopo wa Makundi Maalumu (4.4.2).

# MAFANIKIO YA AFISI YA RAIS, KAZI, UCHUMI NA UWEKEZAJI (UCHUMI NA UWEKEZAJI)



**NDG. HABIBA HASSAN OMAR**
**Katibu Mkuu (Uchumi na Uwekezaji) Afisi ya Rais, Kazi Uchumi na Uwekezaji**

Kwa kuongezea mafanikio yaliyopatikana katika Afisi ya Rais, Kazi, Uchumi na Uwekezaji kwa kipindi cha miezi sita Aprili hadi Septemba 2023.

Kwa upande wa Sekta ya Uwekezaji, sekta ambayo ina umuhimu mkubwa katika kukuza uchumi na kuleta maendeleeo nchini.

Afisi imefanikiwa kuratibu vikao mbalimbali na wawekezaji wa Kampuni tofauti ambao wameonesha nia ya kuwekeza nchini mkwa mfumo wa "Public and Private Partnership (PPP)" miongoni mwa Kampuni hizo ni Enptrol, Meva finance, Elysium health care, Renewable access, Mobile Africa, Yasa consultancy na Elsewedy Electric. Kampuni hizo ziko katika hatua ya kuandaa maandiko ya awali ya miradi ambayo yatawasilishwa katika Taasisi husika.

Aidha, Afisi imefanikiwa kufanya uchambuzi wa mradi wa Pongwe wenye lengo la ujenzi wa nyumba za makaazi. Mradi wa bandari ya abiria inayotarajiwa kujengwa katiak eneo la Maruhubi uliowasilishwa na Kampuni ya ZF Devco, mradi huo kwa sasa ipo GNT kwa kufanyiwa tathmini zaidi.

Kwa Kipindi cha miaka mitano 2023/2027 Afisi imepanga kufanya uchambuzina maandiko ya awali ya miradi ya upembuzi yakinifu ya wa awali ya miradi ya PPP kwa maendeleo ya Taifa pamoja na kuandaa taarifa fupi za miradi (project profile).

Aidha, Afisi imefanikiwa katika kuzitangaza fursa za uwekezaji kwa nchi mbalimbali ili kuweza kutangaza fursa zilizopo katika masuala ya kilimo, uchumi wa buluu, viwanda, ujenzi n.k zikiwemo nchi za Urusi ,China n.k.

Pamoja na hayo Afisi imefanikiwa kuweka miundo mbinu bora kwa ajili ya kuvutia wawekezaji nchini ikiwemo usimamizi wa ujenzi wa barabara katika eneo la Micheweni – Pemba chini ya Kampuni ya Iris Construction and Trade Ltd.

Vilevile, Afisi imefanya mazungumzo na Mabalozi mbalimbali wa Tanzania wanaowakilisha nchi za Uingereza, China, Saudia, Qatar, Burundi Oman, Canada , Australia, Namibia na Ufaransakwa lengo la kuzitangaza fursa na vivutio vilivyopo nchini katika nchi hizo.

Afisi imefanikiwa kutiliana saini wa hati za makubaliano na Kampuni ya Iris Construction Trade Limited ya Uturuki ikiwemo ujenzi wa barabara ya Micheweni – Pemba .

Afisi pia imefanikiwa katika kuunganisha jumla ya Taasisi kumi na moja kutoka Serikalini ambazo zinafanya kazi kwa pamoja na Mamlaka ikiwemo ZRA, TRA, Uhamiaji, Kamisheni ya Ardhi, Kamisheni ya Kazi, Wakala wa Majengo ZBA,Mamlaka ya Uhifadhi wa Mazingira ZEMA, Usajili wa Makampuni ZBPRA, Kamisheni ya Utalii, Idara ya Mipango miji DCU, na Benki ya Watu wa Zaznibar (PBZ) kwa ajili ya kurahisisha utoaji wa huduma za uwekezaji.

Kwa Kipindi cha miaka mitano 2023/2027 Afisi imepanga kutembelea miradi mbalimbali ya uwekezaji inayohitaji kuidhinishwa na Serikali pamoja na kufanya ziara za kutembelea maeneo ya miradi kwa ajili ya kupitishwa miradi hio kwa Unguja na Pemba.

Hata hivyo, Afisi imepanga kufanya ufuatiliaji wa miradi mbalimbali iliyopo Pemba kwa ajili ya kuona namna bora ya uendeleaji wa miradi hio ikiwemo maeneo ya Micheweni.

Afisi imepanga kushiriki katika midahalo, makongamano ya biashara na maonesho ya ndani na nje kwa ajili ya kutangaza fursa za uwekezaji zilizopo nchini pamoja na kuweza kutatua changamoto mbalimbali zinazohusiana na masuala ya uwekezaji.

Afisi imepanga pia kuandaa vikao mbalimbali vya "one stop centre" kwa ajili ya kukaa pamoja ili kutatua changamoto mbalimbali zinazoikabili kuwatengenezea mazingira bora na rafiki wawekezaji kwa kufanya marekebisho ya sheria ili uwekezaji nchini kwa maendeleo ya Taifa.



*Waziri wa Nchi- Afisi ya Rais, Kazi, Uchumi na Uwekezaji Mhe. Mudrik Ramadhan Soraga akiongoza kikao cha kujadili uimarishaji wa Miundombinu ya kiteknolojia nchini ili kufikia adhma ya serikali ya kuifanya Zanzibar kuwa kituo cha Teknolojia Barani Afrika*.

# ZIPA KATIKA KUKUZA UWEKEZAJI NCHINI



*Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Dk. Hussein Ali Mwinyi akizindua Muongozo wa Uwekezaji na Mfumo wa Kieletroniki wa Uwekezaji (ZIPA) katika hoteli ya Golden tulip Uwanja wa Ndege Zanzibar.*

Mamlaka ya kukuza Uwekezaji Zanzibar (ZIPA) ni Taasisi ya Serikali ambayo ipo chini ya Afisi ya Raisi, Kazi, Uchumi na uwekezaji inayofanya kazi zake kwa mujibu wa Sheria nambari 14 ya mwaka 2014 ambayo imeipa mamlaka Taasisi hiyo kushajiisha uwekezaji wa Ndani na Nje kwa kuzingatia Sera ,Miongozo na Ilani ya Chama cha Mapinduzi na kuishauri Serikali juu ya Mikakati sahihi itakayowezesha kuendeleza biashara na kutoa huduma bora kwa Uwekezaji.

ZIPA inakazi ya kuishauri Serikali juu ya sera na mikakati sahihi ya kujenga taswira nzuri ya nchi itakayowezesha kuendeleza biashara, na kutoa huduma bora kwa wawekezaji.

Katika kazi zake za kawaida ZIPA inafanya kazi kama kituo kimoja cha uwekezaji kwa kushirikiana na taasisi tofauti ambazo moja kwa moja zinatoa huduma kwa wawekezaji.

## MAENEO HURU YA UWEKEZAJI

Serikali imetenga maeneo maalum ya uwekezaji ambayo yapo Kisheria kwa Unguja na Pemba kama vile; Eneo la Biashara; Viwanda; Bandari huru; Eneo la Teknolojia ya Habari na Mawasiliano; Eneo la Sayansi na Teknolojia; Eneo La Kilimo; Eneo la Mifugo; Eneo la Uvuvi; Eneo la Utalii na Eneo la Bandari Huru.

Kwa sasa Taasisi hiyo imepewa dhamana na Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kusimamia maeneo matano ya kiuchumi ambayo ni; ; eneo la viwanda vidogo vidogo Amani ambalo linaukubwa wa hekari 12.6 lililoekezwa miradi ya kuzalisha maji, vifaa vya umeme, uzalishaji na ufungaji wa vyakula; eneo huru la uchumi Fumba ambalo linaukubwa wa hekari 3,000 eneo la Micheweni ambalo lina ukubwa wa hekari 808.8 ambalo limetengwa kwa ajili ya uwekezaji wa nyumba za makaazi, malazi, viwanda na Tehama; eneo la Uwanja wa ndege (Amani Abeid Karume Airport) ambalo linaukubwa wa hekari 5 lililotengwa kwa ajili ya uwekezaji wa "logistic park" na eneo la Maruhubi ambalo linaukubwa wa hekari 5.6

*INAENDELEA UKURASA WA 10*




*Makamo wa kwanza wa Rais Mhe. Othman Masoud Othman akiwa katika picha ya pamoja na viongozi wa Serikali na wawekezaji mbali mbali baada ya kufungua kongamano la Biashara na Uwekezaji lililoandaliwa na Mamlaka ya Kukuza Uwekezaji Zanzibar (ZIPA) kwa Usirikiano na Ubalozi wa Marekani (US) lenye lengo la kutangaza na kujadili fursa za Uwekezaji zilizopo nchini.*

Kwa mujibu wa Sheria, Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi amepewa Mamlaka ya kutangaza kupitia gazeti Rasmi Eneo jengine lolote Unguja na Pemba kuwa ni Eneo Huru la Uchumi na anaweza kuidhinisha mipaka au kuyapa majina maeneo hayo. Ardhi yoyote iliyotangazwa kuwa eneo huru la uchumi haitotumika kwa matumizi binafsi.

## KITUO KIMOJA CHA UTOAJI WA HUDUMA ZA UWEKEZAJI ZANZIBAR (ONE STOP CENTRE)

Mamlaka inajukumu la kusimamia kituo kimoja cha kutoa huduma kwa wawekezaji ambacho kina mpa fursa Muwekezaji kupitisha maombi yake yoten yakiwemo maombi ya vibali vya kazi na ukaazi, leseni pamoja na huduma nyengine za lazima zinazohitajika. “One Stop Center” imejumuisha Taasisi 11 kutoka Serikalini ambazo zinafanya kazi kwa pamoja na Mamlaka ya Kukuza Uwekezaji Zanzibar, Taasisi hizo ni; ZRA, TRA, Uhamiaji, Kamisheni ya Ardhi, Kamisheni ya ya Kazi, Wakala wa Majengo ZBA, Mamlaka ya Uhifadhi wa Mazingira ZEMA, Usajili wa Makampuni ZBPRA, Kamisheni ya Utalii, Idara ya Mipango miji DCU na Benki ya Watu wa Zaznibar (PBZ).

## HALI YA UWEKEZAJI NCHINI

Jumla ya miradi 255 imesajiliwa katika kipindi cha miaka mitatu ya uongozi wa Serikali ya awamu ya nane yenye thamai ya mitaji ya dola za Kimarekani 3.7 bilioni amabyo ni sawa na Shilingi 9.2 trilioni za Kitanzania na kutegemewa kutoa Ajira 14,600 kwa Unguja na Pemba. Miradi hiyo inahusiana na masuala ya elimu, viwanda, kilimo na uvuvi, umeme na gesi, ujenzi, afya na shughuli nyengine za kijamii.

## MALENGO YA BAADAE

Taasisi hiyo inategemea kukumilisha mfumo Kielektroniki wa maombi ya Uwekezaji kwa kuziunganisha Taasisi zote zinazohusiana na masuala ya uwekezaji (one stop center) kwa lengo la kupunguza urasimu na muda wa kupata cheti cha uwekezaji na vibali vyengine vinavyohusiana na uwekezaji, mfumo ambao utamuwezesha Muwekezaji kufanya maombi ya Uwekezaji popote alipo Duniani.

# UJASIRIAMALI NI AJIRA



***Waziri wa Nchi,Afisi ya Rais, Kazi, Uchumi na Uwekezaji akikagua mabanda la wajasiriamali katika hafla ya Maadhimisho ya Siku ya Ushirika Duniani yaliyofanyika katika Ukumbi wa Ziwani Mkoa wa Mjini Magharib Unguja.***

Ujasiriamali ni ajira ambayo inatokana na misingi ya utayari pamoja na maandalizi mazuri ambayo yataiwezesha jamii kuweza kuzifikia fursa zilizopo na kutimiza malengo yake na kujikwamua na umasikini nchini.

Tafiti nyingi zinaonesha kuwa kuna changamoto ya ajira duniani ambayo inahitaji kufanyiwa kazi ili iweze kuleta tija na manufaa zaidi hasa kwa vijana kwa kuwaandaliwa mazingira ya uwezeshaji na kuwatafutia mbinu, ujuzi na maarifa katika masuala ya ujasiriamali ili waweze kujikwamua na umaskini.

Kwa mujibu wa viwango vya kazi vya kimataifa ya mwaka 2019 asilimia 27.4 ya vijana wanakabiliwa na changamoto ya kukosa ajira.

Katika kufikia hatua hiyo Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kwa makusudi imeanzisha Wakala wa Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi Zanzibar chini ya Sheria nambari 2 ya mwaka 2022 kwa lengo la kuendelea kuwainua wananchi kiuchumi kwa kuweka mazingira rafiki ya kuwawezesha kufikia lengo la kuinua kipato chao na kupunguza kiwango cha

**MIUNDOMBINU YA UJASIRIAMALI**

Uwezeshaji wananchi kiuchumi unaenda sambamba na uwepo wa miundombinu rafiki na wezeshaji. Katika kulitekeleza hilo Serikali kupitia Afisi ya Rais, Kazi, Uchumi na Uwekezaji imefanikiwa kwa kiasi kikubwa kwa uanzishwaji wa Kituo cha Kulea Wajasiriamali Zanzibar (ZTBI) kilichopo Mbweni – Unguja, Kituo cha Usarifu wa Asali Kizimbani –Unguja, Kituo cha Usarifu wa Asali Pujini - Pemba na Kituo cha Kulea Wajasiriamali Kizimbani (SMIDA) .

Vituo vyote hivi vinafanya kazi ya kutoa mafunzo na kuwalea wajasiriamali katika kazi za uzalishaji wa bidhaa na huduma wanazozitoa ili kufikia malengo yao.

**FAIDA ZA UJASIRIAMALI**

Wakala wa Uwezeshaji wananchi Kiuchumi kupitia kituo cha ZTBI Mbweni imetoa mafunzo... INAENDELEA UKURASA WA 12

*INATOKA UKURASA WA 11*

.....mbali mbali ambayo yamewawezesha wajasiriamali kutangaza bidhaa zao pamoja na kupata ujuzi mpya na endelevu ambao umewasaidia katika kuongeza kipato chao, mafunzo hayo ni kama vile usarifu wa mazao, uokaji na mafunzo ya kidijitali. Aidha,Shirika la Chakula Duniani (FAO) limetoa mashine 18 za usarifu wa mazao na matunda kwa ajili ya kuwasaidia wajasiriamali kuzalisha bidhaa zenye ubora.

Kwa upande wa Kituo cha Barefoot collage kilichopo Kibokwa Kinyasini Unguja kimetoa mafunzo kwa kina mama (Solar mama) jinsi ya kutengeneza vifaa vya umeme wa jua na Vituo vya Kizimbani na Pujini vimetoa mafunzo ya kusarifu asali. Mafunzo hayo yalikuwa na lengo la kuwasaidia wajasiriamali katika kuzalisha bidhaa zenye ubora na kuweza kupata masoko ya uhakika ya Ndani na Nje ya Nchi, Jumla ya wajasiriamali1615 wamepatiwa mafunzo hayo, wajasiriamali 750 wamepatiwa vifaa vya kisasa vya ufugaji wa nyuki na wajasiriamali 753 wamepata mafunzo ya ufuigaji wa nyuki.

Wajasiriamali wamepata mitaji ya TZS. 21,730,733,292.4 kupitia mikopo ya Uviko 19 na Mfuko wa Khalifa, kwa upande wa Mfuko wa Inuka jumla ya TZS. 19,635,733,292.40 zimetolewa (Unguja TZS.11,842,120,608 na Pemba ni TZS.7,793,612,684.20) ambapo kwa sasa jumla ya wanufaika wa mikopo hio ni 19,109 (Unguja 9,440 na Pemba 9,669) kati ya hao Wanaume ni 7,424

Wajasiriamali wamepata mitaji ya TZS. 21,730,733,292.4 kupitia mikopo ya Uviko 19 na Mfuko wa Khalifa, kwa upande wa Mfuko wa Inuka jumla ya TZS. 19,635,733,292.40 zimetolewa (Unguja TZS.11,842,120,608 na Pemba TZS.7,793,612,684.20) ambapo kwa sasa jumla ya wanufaika wa mikopo hio ni 19,109 (Unguja 9,440 na Pemba 9,669) kati ya hao Wanaume ni 7,424 na Wanawake ni 11,685. Na kwa upande wa Mfuko wa Khalifa jumla ya TZS. 2,095,0000,000 (Unguja 1,855,000,000 na Pemba 2,400,000,000) zimeshatolewa kwa miradi 18 (Unguja 16 na Pemba 2)

Kuwepo kwa fursa ya upatikanaji wa masoko ya bidhaa za Ndani na Nje ya Nchi kwa makubaliano na Taasisi mbali mbali zinazotoa fursa kwa wajasiriamali kama vile; Tantrade, Maisha Bora Foundation, USAID na Shirika la Viwango Zanzibar- ZBS.

Kutokana na umuhimu wa uwepo wa wajasiriamali Nchini, Serikali imeunda Taasisi inayosimamia Vyama vya Ushirika chini ya Sheria nambari 15 ya Mwaka 2018 ambayo imesaidia kuviunganisha Vyama hivyo na Serikali ili kuleta mafanikio kwa wanaushirika na Taifa kwa ujumla. Jumla ya vyama vya Ushirika 579 vimesajiliwa Unguja na Pemba vinavyojishughulisha na kazi mbali mbali ikiwemo uanikaji wa dagaa, kilimo, utalii, huduma za simu na kazi nyengine za mikono . Taasisi imetoa mafunzo kwa wanaushirika 1,703 Unguja na Pemba juu ya utafutaji wa masoko, usimamizi wa fedha , upangaji wa bei za bidhaapamoja na utunzaji wa kumbukumbu za hesabu.

Itakumbukwa kuwa kila ifikapo Jumamosi wa mwanzo ya mwezi wa Julai ya kila Mwaka ni Maadhimisho ya Siku ya Ushirika Duniani. Kauli mbiu ya mwaka huu ilikuwa ni" USHIRIKA NI WADAU WA KUHARAKISHA MAENDELEO ENDELEVU"



*Vijana wakiwa katika mafunzo ya upishi wa vyakula vya aina mbalimbali ikiwemo mikate, vileja na keki katika Chuo cha Kukuza na Kulea Wajasiriamali Zanzibar (ZTBI) kilichopo Mbweni Wilaya ya Mjini Unguja*

# UTEKELEZAJI WA SHERIA ZA KAZI ZANZIBAR



*Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Mhe Hussein Ali Mwinyi akimkabidhi cheti cha ufanyakazi bora na pesa taslim mfanyakazi ndugu Khatib Khalid  Hamad kwa niaba ya ndugu Yussuf Ali Mjombo katika Maadhimisho ya Siku ya Wafanyakazi Duniani yaliyofanyika Nungwi , Mkoa wa Kaskazini Unguja*

Kamisheni ya kazi  ipo kwa mujibu wa Sheria namba  11 ya mwaka 2005 ambayo imeundwa rasmin kwa ajili ya kuweka mfumo wa kiutawala na kiutendaji ambayo imepelekea kuimarika kwa sekta ya kazi Zanzibar na kuleta mabadiliko  katika Sheria za kazi na kuzifanya ziendane  na wakati pamoja na viwango vya kazi vya kimataifa.

Kamisheni ya kazi ina fanya kazi zake  chini ya Afisi ya Rais Kazi Uchumi na Uwekezaji pamoja na kushirikiana na Vyama vya Wafanyakazi na Jumuiya za Waajiri (ZATUC na ZANEMA) , kuhakiki mikataba ya wafanyakazi na kuona wafanyakazi wanapata stahiki zao kwa wakati kwa mujibu wa Sheria pamoja na kushughulikia utatuzi wa migogoro katika sehemu za kazi.

Lengo kuu la kuundwa kwake ni kusimamia utekelezaji wa Sheria za kazi na Sera ya Ajira ya Zanzibar pamoja na kuwa na jukumu la kufanya ukaguzi ambayo itasaidia kupatikana ajira za staha na kutatua migogoro katika sehemu za kazi, kuimarisha mahusiano mema kazini, kupinga ajira za watoto , kuimarisha majadiliano ya pamoja kazini, kujenga uwelewa kwa jamii kuhusu sera, sheria za  kazi na ajira pamoja na mikataba ya kimataifa na kikanda inavyohusiana na masuala ya kazi.

Idara hiyo  pia ina muundo wa Idara 3 nazo ni Idara ya Ajira, Idara ya Usalama na Afya Kazini na Kamisheni ambayo inafanya kazi kwa mashirikiano ya karibu na Kitengo cha Usuluhishi na Uamuzi wa Migogoro yaKkazi (DHU) ,Afisi ya Mrajis na Jumuiya za Waajiri, Kitengo cha Kupambana na Ajira za Watoto , Kitengo cha Elimu Kazi na Kitengo cha Mahusiano Kazini na Viwango vya Kimataifa.

Katika kutekeleza maagizo ya Mhe. Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Mhe. Hussein Ali Mwinyi, Waziri wa Wizara hiyo Mhe. Mudrik Ramadhan Soraga kupitia Kamisheni ya Kazi tarehe 24 Machi 2023 aliweza kutangaza ulipaji mpya wa kima cha chini mishahara (Minimum wage) ambacho ni shilingi 347,000 baada ya shilingi 300,000 kwa wafanyakazi wenye hadhi ya mikataba ya maandishi, mshahara mpya kwaTaasisi ndogo (small institution) kuwa ni shilingi 250,000 baada ya shilingi 180,000 kiima cha zamani, wafanyakazi wa wenye mikataba ya masharti ya kutwa wenye ujuzi kima cha kutwa ni shilingi 30,000 na wasio na ujuzi shilingi 25,000. Wafanyakazi wa majumbani kima cha zamzni 80,000 kima kipya ni shilingin 100,000 na shilingi 120,000 kwa wafanyakazi wanaokwenda na kurudi majumbani kwao .

Aidha, katika mapendekezo hayo Kamisheni ya Kazi kupitia Bodi hiyo imefanikiwa kuandaa mapendekezo ya kima maalum cha mshahara kwa wafanyakazi wa kigeni ambacho ni USD 1000 .

Ili kuona utekelezaji wa maagizo hayo Kamisheni ya Kazi ililazimika kufanya ukaguzi maalum wa ufatiliaji wa ongezeko la kima cha mishahara hiyo ambapo ilifanikiwa kufanya ukaguzi kwa taasisi 35 na kubaini kuwa taasisi 25 ndizo zilizoweza kua anza kutekeleza agizo hilo na 10 bado hazijaanza kulipa kutokana na upya wa taasisi zao , na nyengine kutokuwa na uwezo wa kulipa na kuleta maombi katika idara ya kamisheni na mpaka sasa tayari maombi yao yameshaaza kufanyiwa kazi.

Kwa upande wa Fao la Upotevu wa Ajira ambalo linalipwa kutokana na mashirikiano yaliyopo baina ya ZSSF na Kamisheni ya Kazi iliingia Mkataba wa Makubaliano ( MoU ) kwa ajili ya ulipaji wa fao hilo mnamo mwezi Machi 2023. Kwa kipindi cha mwezi wa nne hadi sasa Kamisheni imeweza kutoa madodoso 257 kwa Unguja na Pemba 105 kwa lengo la kupata taarifa mbalimbali za Wafanyakazi na waajiri kwa upande wa Sekta Binafsi (Private Sectors ).

## MAFANIKIO

Kwa Kipindi cha Aprili hadi Septemba 2023 Idara hiyo imeweza kufanya ukaguzi kwa taasisi 151 kwa Unguja 83 na Pemba 68 ukaguzi huo ulifanyika kwaajili ya kuangalia Sheria za kazi kwa Taasisi Binafsi kama zinatekelezwa ambazo zilihusisha mahoteli , viwanda , sehemu za kilimo ,ujenzi nk.

Pia Idara imeweza kutoa vibali vya kazi kwa wafanyakazi wa kigeni 1508, waliopata msamaha kwa Mhe. Waziri ni 77, waliopata msamaha ZIPA 80, vibali vipya ni 4,010, vibali vilivyoengezewa muda 582 na vya muda mfupi ni 341 vyote ni kutoka katika mataifa mbali mbali ikiwemo Zambia ,German, Yemen, American , Sudan, Canada nk.

Vile vile imeweza kudhibitisha mikataba ya kazi kwa wafanyakazi wazawa 8684 Unguja na Pemba kwa upande wa Unguja ni 7,777 na kwa Pemba ni 907. Aidha mikataba yote hiyo ilithibitishwa kwa wafanyakazi kama inaendana na Sheria za kazi.

Kwa upande wa usuluhisi na uamuzi wa migogoro ya kazi migogoro iliyo wasilishwa ni 136, iliyomalizika kwenye usuluhishi ni 18, inayoendelea katika hatua za uamuzi ni 52, migogoro inayoendelea katika usuluhishi ni 58 na iliofanikiwa kumaliza ni 7.

Kamisheni ya kazi imefanikiwa kuandaa kanuni mpya tatu (3) (kanuni ya kuchukua wanafunzi kwa vitendo, kanuni ya Raia wa kigeni wanaofunga ndoa na Wazanzibar na kanuni ya kumaliza makosa) kanuni ambazo zinatarajiwa kurahisisha utekelezwaji wa Sheria za kazi kwa ufanisi.

INAENDELEA UKURASA WA 15

Aidha , Kamisheni ya Kazi imefanikiwa kuijengea uwezo Kamati ya utatu ( Tripartite Committee) kwa kuwapatia wajumbe wake mafunzo maalum ya kazi za kushauri masuala ya usuluhishi na utatuzi wa migogoro ya kazi.

Pia, Kamisheni ya Kazi imefanikiwa kuwasilisha mapendekezo ya kufutwa kwa Sheria ya Ajira nambari 11 ya 2005 na kuanzishwa Sheria mpya ya Kazi na Ajira ya 2023 katika kikao cha Makatibu Wakuu na tayari Makatibu Wakuu wameshatoa maoni yao ambayo Kamisheni inafanya kazi ili hatua stahiki ziweze kufuata.

Mbali na hayo, Kamisheni ya Kazi kwa kushirikiana na Ofisi ya Waziri Mkuu, Kazi, Ajira na wenye Ulemavu kwa pamoja na Washirika na wadau mbalimbali wa mambo ya kazi imefanikiwa kupitia na kuandaa ripoti maalum ya nchi ya utekelezaji wa Miaktaba ya Shirika la Kazi Duniani.

Kwa upande wa Afisi ya Mrajis wa Vyama vya Wafanyakazi na Jumuiya za Waajiri imefanikiwa kusuluhisha migogoro mitatu (3) inayohusu kusimamishwa uanachama wanachama wa Chama cha ZAFICOWU kinyume na Sheria , kusitishwa ada za wanachama wa TEWUTA-Z na ZAPSWU pamoja na kufanya ukaguzi wa Chama cha TUICO katika Tawi la Kampuni ya ujenzi ya Volk House.

## CHANGAMOTO

Pamoja na mafanikio yaliyopatikana kwa kipindi cha miezi sita . Kamisheni inakabiliwa na changamoto mbalimbali ambazo zinakwamisha utendaji wa majukumu yake kwa ufanisi, zikiwemo uhaba wa rasilimali watu, uhaba wa vitendea kazi vikiwemo vyombo vya usafiri kwa ajili ya ukaguzi kazi na ufuatiliaji wa malalamiko ya wafanyakazi, uhaba wa bajeti , kukosa mifumo ya ukusanyaji, uwekaji kumbukumbu na uwenezaji wa taarifa mbalimbali za kazi na kukosekana kwa Mamlaka ya Kamisheni ya Kazi (autonomous) kunaifanya Kamisheni kuwa tegemezi katika utekelezaji wa majukumu yake




*Katibu Mkuu (Kazi na Uwezeshaji),Afisi ya Rais, Kazi, Uchumi na Uwekezaji Bi Maryam Juma Abdulla akiwa pamoja na Mkurugenzi wa Mfuko wa Hifadhi ya Jamii (ZSSF) ndugu Nassor Shaaban wakionesha hati za makubaliano ya Fao la Upotevu wa Ajira baada ya kutiliana saini makubaliano hayo huko Mwanakwerekwe Wilaya ya Mjini.*

# FURSA ZA AJIRA KWA VIJANA



vijana waliojijitokeza katika zoezi la usaili wa nafasi za kazi katika hoteli ya St. Regis Al Mouj iliyopo Nchini Muscut Oman, iliyofanyika katika hoteli ya Serena Shangani Mjini Unguja.



Afisa Ajira ndugu Mohammed Said Khamis akiwa katika zoezi la kuwasomea mikataba ya kazi vijana wanaotarajia kwenda nchini Oman kufanya kazi.

Idara ya Ajira imeundwa kwa kuzingatia kifungu nambari 5.1 cha Sera ya Ajira ya mwaka 2009 ikiwa ni sehemu ya utekelezaji wa sera hiyo amabyo ina jukumu la kukuza na kuimarisha uchumi wa Nchi; Kuimarisha na kukuza ujuzi kwa Vijana ili waweza kujitegemea kwa kuwa na uwezo wa kuajirika na kujiajiri wenyewe; Kubuni na kusimamia Mpango na taratibu za soko la Ajira na kuhakikisha kuwa fursa za ajira zinapatikana kwa usawa na kwa wote; Kuanzisha na kusimamia mfumo wa ukusanyaji, uchambuzi na uwekaji wa taarifa za Soko la Ajira; Kukusanya na kuchambua taarifa za Soko la Ajira pamoja kuratibu shughuli za Uwakala Binafsi wa Ajira.

Afisi ya Rais, Kazi, Uchumi na Uwekezaji kwa kushirikiana na Shirika la Kazi Duniani (ILO) imeanzisha Programu mbalimbali zenye lengo la kutoa mafunzo kwa Vijana ili kuweza kuwajengea uwezo wa kujiajiri na kuajirika, programu hizo ni kama vile; Apprenticeship; Internship na Modular Apprenticep.

Katika kipindi cha Aprili hadi Septemba, 2023 Taasisi imesimamia programuya kujenga uzoefu wa kazi kwa Vijana (Intership), ambapo Vijana 50 (wanaume 21 na wanawake 29) wamepata mafunzo ya kuwaandaa na kuwajengea uwezo wa kujiamini katika kufanya kazi zao katika fani ya hotelia, ufundi gereji, ualimu na ushoni.

Vile vile, imeratibu na kusimamia Mawakala Binafsi wa Ajira ambao wana jukumu la kuwasajili watafuta kazi na kuwaunganisha na Ajira za Staha, katika kipindi cha miezi sita jumla ya Taasisi mpya mbili zilizotimiza vigezo zimesajiliwa ambazo ni Sashamark na Mahasna na kuzifanyia ukaguzi Taasisi nne zinakusudia kuongeza muda wa leseni ili ziweze kuendelea na shughuli zao ambazo ni Taasisi ya IBS Zanzibar Limited, Afnan Recruitment Agency na Blue Ageny Company Limited na Dejure Attorney. Hivyo, kwa sasa kuna jumla ya Taasisi za Uwakala Binafsi wa Ajira kumi na nane (18).

## MAFANIKIO

Kwa kushirikiana na Wakala Binafsi wa Ajira Afisi imeratibu upatikanaji wa Ajira za Staha Nje ya Nchi kwa Vijana 612 (Wanawake 493 na Wanaume 119), katika kazi za udereva, kazi za majumbani, na vibarua ikiwemo vibarua vya ujenzi na kusambaza mizigo katika Nchi za Oman, Qatar, Saudi-Arabia na Visiwa vya Sheli sheli.

Vijana waliopatiwa fursa za Ajira Nje ya Nchi wamefanikiwa kwa kuweza kujikimu kimaisha ikiwemo kusomesha Watoto na kuendeleza familia zao .

## CHANGAMOTO

Kuwepo kwa baadhi ya Mawakala ambao hawajasajiliwa na hawana vigezo wanaofanya udanganyifu na kufanya kazi za uwakala kinyume cha Sheria ya Ajira.

Baadhi ya wafanyakazi wanaokwenda Nje ya Nchi wanakatisha muda wa mikataba ya kazi, wanafanya udanganyifu wa vipimo vya afya , kima cha mishahara wanachopewa kwenda kinyume na makubaliano ya mikataba na kutokuwa na uzoefu wa kufanya kazi.

# IFAHAMU OSH – ZANZIBAR

Uwekezaji katika Rasilimali watu ni jambo muhimu ambalo linasaidia katika kuekeza na kuimarisha masuala ya afya na usalama katika maeneo ya kazi iwapo litazingatiwa na kutiliwa mkazo katika kuimarisha afya za wafanyakazi katika sekta mbali mbali.

Kwa kuzingatia kuzingatia suala hilo, Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar imeanzisha Idara ya Usalama na afya




*Afisa Mkaguzi Usalama Kazini ndugu Said Bakar Khamis akifanya ukaguzi wa jenerata la Taasisi ya Mfuko wa Hifadhi ya Jamii (ZSSF) iliyopo Kilimani Wilaya ya Mjini.*

Afya Kazini kwa mujibu wa Sheria nambari 8 ya mwaka 2005 ikiwa na lengo la kuimarisha afya za wafanyakazi kwa kufanya ukaguzi katika maeneo ya kazi; kutoa maelekezo na ushauri kwa Taasisi za Umma na Binafsi kwa kuzitambua, kuzisajili na kuweka kumbukumbu za usalama kwa mujibu wa viwango vya Kitaifa na Kimataifa pamoja na kuandaa mazingira rahisi ya kazi.

Kila ifikapo tarehe 28 Aprili ya kila mwaka ni Maadhimisho ya Siku ya Usalama na Afya Kazini ambapo ujumbe wa mwaka huu ulikuwa ni "MAZINGIRA SALAMA YA KAZI NA YENYE AFYA NI KANUNI YA MSINGI NA HAKI YA KILA MUAJIRI NA MUAJIRIWA KATIKA KAZI"

Afisi imetia saini Hati ya Mashirikiano na Wakala wa Usalama Mahala Pa Kazi (OSHA) pamoja na kufaya ziara ya mashirikiano katika Ofisi ya Waziri Mkuu, Kazi, Vijana,Ajira na Wenye Ulemavu huko Tanzania Bara kwa lengo la kuwajengea uwezo wafanyakazi wake katika mafunzo ya muda mrefu na muda mfupi, kubadilishana uzoefu juu ya mfumo wa usimamizi wa usalama na afya kazini pamoja na kuiimarisha programu katika utekelezaji wa majukumu yake.

## MAFANIKIO

Kwa kipindi cha miezi Sita, Aprili hadi Septemba, 2023 programu imefanikiwa kufanya ukaguzi katika Taasisi za Umma na Binafsi 90 (44 Ungujana 46 Pemba) na kuwashauri waajiri kuweka mifumo mizuri na mazingira bora ya kazi ili kujiepusha na matukio ya ajali na maradhi yasiendelee katika sehemu za kazi.

Imefanikiwa kusajili sehemu 28 (19 Unguja na 9 Pemba) kwa lengo la kuzitambua na kuzifahamu zilipo pamoja na kazi wanazojishughulisha nazo ili kuweza kuwafanyia tathmini za hatari zinazoweza kutokea katikamaeneo yao ya kazi.

Imefanya uchunguzi wa matukio 3 ya ajali na maradhi yaliyoripotiwa katika sehemu za kazi wakati wafanyakazi wakiendelea na majukumu yao, ajali hizo ni;

1.Ajali ya moto ambayo ilihusishwa na chanzo cha kemikali kutoka maabara ya Skuli ya Langoni Wilaya ya Maghribi A.

Ajali ya kuzama kwa mtoto na kufariki dunia katika bwawa la kuogolewa la Abla Beach Apartment ilioko Beit –el-Raas Wilaya ya Maghrib A iliyosababishwa na kuteleza na kuanguka katika bwawa hilo.

Ajali ya moto ulioharibu mali zote katika hoteli 5 za kitalii ambazo ni The Nest, Meraki, Cristal, Mambo, Matamna na Drifters zilizotokea Paje Wilaya ya Kusini Unguja.

Imetoa mafunzo kwa wawakilishi 130 Unguja na Pemba wa usalama na afya kazini kutoka katika Taasisi za Umma na Binafsi pamoja na kuwafahamisha majukumu yao na wanachotakiwa kufanya wakiwa katika majukumuhayo.

Aidha, imeratibu mkutano mmoja Pemba wenye lengo la kujadili kanuni 3 zinazotoa ufafanuzi wa Sheria nambari 8 ya mwaka 2005 ya Usalama na Afya Kazini juu ya masuala ya huduma ya kwanza (Fast Aid) uliowashirikisha wadau kutoka Taasisi mbalimbali.

INAENDELEA UKURASA WA 17

Inatoka ukurasa wa 16

# CHANGAMOTO

Baadhi ya changamoto zilizojitikeza katika utekelezaji wa program hii ni Pamoja na; uhaba wa vitendea kazi ambavyo vinajumuisha vifaa vya ukaguzi na uchunguzi wa usalama na afya kazini, uhaba wa watendaji wenye utaalamu mahsusi wa masuala ya afya, wahandisi mitambo na maafisa saikolojia.

Mbali na changamoto hizo lakini idara hiyo imejiwekea mikakati mbali mbali ikiwemo kupitia wahisani amabo mwatasaidia katika upatikanaji wa vifaa vya ukaguzi na uchunguzi wa ajali za Usalama na Afya Kazini.

Kuhusu suala la uhaba wa wataalamu tayari wameshapeleka maombi katika Tume ya Utumishi Serikalini kwa ajili ya kupatiwa watendaji wenye utaalamu wa masuala ya afya, wahandisi mitambo, maafisa saikolojia n.k.



*Mkurugenzi wa Idara ya Usalama na Afya Kazini Dkt. Ali Said Nyanga akiwa pamoja na watendaji kutoka katikaidara hiyo akimpa maelekezo ya usalama na afya katika sehemu za kazi Bw. Othman Yussuf, kutoka katika kampuni ya Orkun inayojishuhulisha na ujenzi wa barabara ya Mangapwani yenye kilomita kumi na Mbili, baada ya kufanya ziara ya kutembelea na kukagua eneo hilo.*



*Mfanyakazi kutoka Afisi ya Rais, Kazi, Uchumi na Uwekezaji Bi Hindi Said Shindano akiwa katika zoezi la upimaji wa macho na Dakatari kutoka Wakala wa Usalama Mahala Pa Kazi Tanzania bara uliofanyika Afisini Mwanakwerekewe Wilaya ya Magharibi B.*

# USHIRIKIANO WA SEKTA YA UMMA NA SEKTA BINAFSI KATIKA UWEKEZAJI




***Waziri wa Nchi, Afisi ya Rais, Kazi, Uchumi na Uwekezaji Mhe. Mudrik Ramadhan Soraga akiwa katika picha ya pamoja na Kamishna kutoka Idara ya Mashirikiano baina ya Sekta za Umma na Sekta Binafsi Dkt. Bill Kiwia na Menaja Uchumi kutoka Bewnki Kuu ya Tanzania (BOT) ndugu Moto Lugobi katika hafla ya kukabidhiwa leseni Kampuni ya Airpay Tanzania pamoja na ufunguzi wa ofisi za Kampuni hiyo huko Mlandege Wialaya ya Mjini.***

Idara ya Mashirikiano baina ya Sekta ya Umma na Sekta Binafsi (PPP) ipo chini ya Afisi ya Rais Kazi Uchumi na Uwekezaji kwa mujibu wa Sheria namba 8 ya mwaka 2015 ikiwa na lengo la kutoa huduma na kuruhusu sekta binafsi kuweza kushirikiana na sekta za Serikali katika mambo mbali mbali ya maendeleo.

## DHANA YA PPP

PPP ilianza katika mfumo wa miradi ya maridhiano iliyosimamiwa na Sheria ya Maridhiano (Project Concession Act NO. 9) ya Mwaka 1999 ambayo ilionekana kuwa na mapungufu mengi katika utekelezaji wake na kuonekana kuwa kuna umuhimu wa kuwepo mfumo wa kisheria na kitaasisi utakaosimamia miradi ya PPP.

Idara ya PPP ilianzishwa mwaka 2012 kwa lengo la kuratibu na kusimamia miradi yote ya mashirikiano baina ya Sekta za Umma na Wawekezaji. Hatua ambayo ilitoa muelekeo kwa Serikali hususani katika miradi ya PPP na katika maeneo ya uwekezaji

Miongoni mwa sababu kuu zilizopelekea kuundwa kwa Idara hii ni pamoja na; Kuimarisha uchumi wa Nchi; Kuongeza pato la Taifa, kupanuwa wigo wa uwekezaji kutokana na miundombinu iliyopo ya utoaji huduma kwa umma na kwa jamii kwa ujumla pamoja na kuongeza ubunifu na ufanisi katika utekelezaji wa miradi hiyo .

Kwa mujibu wa Sera, Sheria na Kanuni, Miradi yote ya PPP ni lazima izingatie mambo yafuatayo; Thamani ya kifedha; maslahi kwa umma; uwazi na uwajibikaji katika mchakato wa miradi ya PPP; Ushindani; mgawanyo wa vichocheo hatarishi; kulenga matokeo ya mazingira na mabadiliko ya tabia nchi pamoja na ufuatiliaji na tathmini.

*INAENDELEA UKURASA WA 19*

# USHIRIKIANO WA SEKTA YA UMMA NA SEKTA BINAFSI KATIKA UWEKEZAJI

## MAFANIKIO YALIYOPATIKANA KUPITIA MIRADI WA PPP

Miongoni mwa mafanikio yaliyopatikana kupitia Miradi iliyowekezwa kwa njia ya PPP ni Pamoja na; Kukuza uchumi wa Nchi; Kuimarika kwa huduma za miundombinu; Kuongezeka kwa uwekezaji katika miundombinu, kuongezeka kwa fursa za ajira na huduma za jamii Pamoja na Kuhifadhi na kulinda mazingira na urithi wa Zanzibar.

Programu imeratibu uchambuzi wa Kisheria na mazingira ya kijamii kwa miradi ya PPP na kuanzisha mfumo wa kuratibu malalamiko kwa waathirika wa miradi hiyo .

Imefanikiwa kuanzisha kwa tawi la Idara ya hiyo Pemba kwa ajili ya kushughulikia miradi kwa Pemba pamoja na kufanya ziara katika Idara ya PPP Tanzania bara kwa lengo lakupeana uzoefu na kuwa na mashirikiano mazuri baina ya Zanzibar na Tanzania bara.

## CHANGAMOTO WANAZO KUTANA NAZO

Changamoto zilizojitokeza katika miradi ya PPP ni pamoja na Uwelewa mdogo kwa jamii juu ya dhanaya uwepo wa PPP; Upungufu wa fedha katika utayarishaji wa miradi; Uwezekano wa kutokea rushwa wakati wa zabuni na Uchafuzi wa mazingira wakati wa ujenzi na utekelelezaji wa miradi endapo hatua za udhibiti hazitochukuliwa na kutokuwepo kwa mashirikiano mazuri baina ya sekta husika na Idara ya Mashirikiano Baina ya Sekta ya Umma na Sekta Binfasi.

**Tanbihi:** PPP sio suluhisho la utekelezaji wa miradi yote ya maendeleo kwani si kila mradi unaweza kutekelezwa kwa mfumo wa PPP.



***Maafisa wa Idara ya Mashirikiano baina ya Sekta za Umma na Sekta Binafsi (PPP) wakiwa katika ziara ya kutembelea eneo la mradi wa machinjio liliopo Kisakasaka Wilaya ya Magharib B.***

# MATUKIO KATIKA PICHA




*Waziri wa Nchi Afisi ya Rais Kazi Uchumi na Uwekezaji Mhe. Mudrik Ramadan Soraga akimkabidhi cheti cha shukrani Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Dkt. Hussen Ali Mwinyi katika uzinduzi wa Mfumo wa Kuhudumia Wawekezaji kielektroniki (Online Services) na Muongozo wa Uwekezaji Zanzibar katika Ukumbi wa Golden Tulip uliopo U/Ndege Zanzibar.*




*Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Dkt. Hussein Ali Mwinyi akiwa katika picha ya pamoja na baadhi ya viongozi wa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar katika Sherehe za Maadhimisho ya Siku ya Wafanyakazi Dunianihuko Nungwi Mkoa Wa Kaskazini Unguja.*



*Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Mhe. Hussein Ali Mwinyi akifungua hoteli ya Emerald Zanzibar and Spa iliyopo Matemwe Mkoa wa Kaskazini Unguja.*

YANAENDELEA UKURASA WA 21 NA 22

KUTOKA UKURASA WA 20




*Waziri wa Nchi Afisi ya Rais Kazi Uchumi na Uwekezaji Mhe. Mudrik Ramadan Soraga akimkabidhi Ndg. Abubakar Aziz Meneja wa Kampuni ya Azam Marine hati ya utambuzi kwa wawekezaji wa kimkakati katika Ukumbi wa Ofisi za ZIPA Maruhubi Unguja.*




*Mkurugenzi wa Mfumo wa Fao la Upotevu wa Ajira kutoka ZSSF ndugu Khatib Iddi Khatib akiwakabidhi kifaa cha kufanyia kazi (computer) Katibu Mkuu (Kazi na Uwezeshaji) Bi Maryam Juma Abdalla pamoja na Kamishna wa Kazi ndugu Rashid Khamis Othman kwa ajili ya matumizi ya Mfumo wa Fao la waliopoteza ajira.*



*Viongozi wa Afisi ya Rais Kazi Uchumi na Uwekezaji wakiwa katika picha ya pamoja baada ya kumaliza ziara ya ukaguzi wa Mradi wa Ujenzi wa Miundombinu ya Barabara Maeneo huru ya Uwekezaji Micheweni Pemba.*



*Waziri wa Nchi Afisi ya Rais Kazi Uchumi na Uwekezaji Mhe. Mudrik Ramadhan Soraga akimuonesha vifaa vya kuchakatia asali  Waziri wa Ardhi na Maendeleo ya Makaazi Mhe. RahmaKasim Ali  baada ya kufanya ufunguzina  kutembelea kituocha kusarifia zao la  asali kilichopo Kizimbani Wilaya ya Magharibi ''A'' Unguja.*




*Naibu Katibu Mkuu (Kazi Na Uwezeshaji)  Afisi ya Rais Kazi Uchumi na Uwekezaji Bi Halima MaulidSaleh na   wakiwa kwenyepicha ya pamoja na Bwana Maurizio Busatti baada ya kusaini Hati ya Makubaliano baina ya Afisi Ya Rais Kazi Uchumi na Uwekezaji na ShirikaLa Umoja wa Mataifala Uhamiaji  (International For Migration - IOM). Hafla iliyofanyika katika Ukumbi wa Afisi  Mwanakwerekwe Wilaya ya Mgharibi ''B''.*



*Hafla ya Utiaji Sainiwa Hati ya Makubaliano kati ya Wakalawa Usalama Mahala Pa Kazi( OSHA ) Tanzania Bara na Idara Ya Usalama na Afya Kazini ( OSH) Zanzibar.Makubaliano hayo yamefanyika baina yaMkurugenzi Wa OSH Dkt. Ali Saidi Nyanga naMkurugenzi wa OSHA Bibi Khadija Mwenda katika Hoteli ya Golden Tulip iliyopo Uwanja wa Ndege.*




*Waziri wa Nchi Afisi ya Rais, Kazi, Uchumi na Uwekezaji akiwa katika picha ya pamoja na Makamo wa Pili wa Rais Mhe. Hemedi Suleiman Abdallah pamoja na viongozi wengine wa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar katikaMaadhimisho ya Siku ya Ushirika Duniani yaliyofanyika katika Ukumbi wa Ziwani Mkoa wa Mjini Magharibi.*




*Waziri wa Nchi Afisi ya Rais Kazi Uchumi na Uwekezaji Mhe. Mudrik Ramadhan Soraga akimkabidhi vitendea kazi Mwenyekiti wa Bodi ya Uwakala Wananchi Kiuchumi Bw Ameir Juma Mohamed katika uzinduzi wa Bodi yakwanza ya Wakala wa UwezeshajiWananchi Kiuchumi katika ukumbi wa Golden Tulip uliopo Uwanja wa Ndege Wilaya ya Magharib ''B''.*



*Mheshimiwa Dk. Ali Mohamed Shein Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Mstaafu akifungua radi wa Hoteli ya Nyota Tano -TOA Hotel and SPA iliyopo Matemwe  Kaskazini Unguja.*

# WASEMAVYO



*Naitwa Mohammed Haji Ameir. Mjumbe wa Bodi ya Mtule Amcos Ltd iliyopo Paje. Tunajishuhulisha na upandaji na uvunaji wa Tungule, kwa sasa tunachakata tungule na kuzitengenezea Tomato Sauce . Tunawaomba wananchi  kushirikiana nasi kwa kununua bidhaa zetu. Naimani kikundi chetu hichi kitaondoa tatizo la Ajira kwa vijana wapatao 150. Naishukuru Afisi ya Rais, Kazi, Uchumi na Uwekezaji kupitia Idara ya Ushirika kwa uwepo wa Siku ya Ushirika Duniani ambayo imekuwa ni chachu ya Maendeleo kwa Vikundi vya Ushirika- Zanzibar.*



*Naitwa Hamza Kassim Khamis nakaa Mfenesini Mkoa wa Mjini Magharibi, ni mlemavu wa mikono. Naishukuru Serikali kupitia Afisi ya Rais, Kazi, Uchumi na Uwekezaji kwa kushirikiana na Shirika la Kazi Duniani (ILO) kwa kuweza kunipatia fursa ya mafunzo ya muda mfupi (NEET) ambayo yameendeshwa na Skuli ya Kujenga Taifa – Mtoni. Nimesomea fani ya Ushoni (nguo) lakini pia nilipata nafasi ya kujifunza kushona viatu. Mafunzo hayo yamenisaidia kuweza kupata ujuzi ili niweze kujiajiri mwenyewe, naendelea kuishukuru Serikali kwa kuweza kunipatia charahani pamoja na vifaa vyengine ili niweze kujiendeleza katika fani hii. Ujumbe wangu walemavu wapewe.*



*Naitwa Khairat Nassor Salum  ni mwanaafunzi wa Chuo Kikuu cha Taifa Zanzibar – Kampasi ya Kilimani. Naishukuru Serikali kupitia Idara ya Usalama na Afya Kazini kwa kuja katika Chuo chetu kutupatia mafunzo yanayohusiana na usalama na afya katika sehemu za kazi. Nimejifunza vitu vingi ikiwemo kuweza kujua athari mbalimbali zinazoweza kujitokeza katika mazingira ya kazi vilevile anawashauri vijana waombe nafasi za kazi ambazo zinaendana na na afya zao ili kuondoka atahri zinazoweza kujitokeza.*



*Naitwa Said Abdallah Bakhresa , Muwekezaji kutoka Kampuni inayojishughulisha na ujenzi wa nyumba eneo la Fumba. (Fumba Town Living). Naishukuru Serikali kwa kunipatia fursa ya kuwekeza Zanzibar.  Nawashauri wawekezaji wenzangu kuja kuwekeza katika visiwa hivi na kutembelea maeneo mbalimbali zenye vivutio kwa kuitangaza Zanzibar kwa rasilimali zilizopo.*



*Naitwa Sebastian Dietzold ni Mkurugenzi wa Kampuni ya CPS kampuni inayojishuihulisha na ujenzi wa nyumba. Tumeweza kujenga mji wa kisasa Dimani na Nyamazi ambao una maduka ya kisasa, shule, hospitali, maduka n.k. Naishukuru Serikali kupitia ZIPA kwa kuwapatia nafasi ya kuwekeza katika Zanzibar ili kuwaletea wananchi mazingira mazuri ya makaazi.*

# WADAU WETU

CRDB BANK

THE PEOPLE'S BANK OF ZANZIBAR LIMITED
PBZ IKHLAS
PBZ BANK

NMB

Tanzania Commercial Bank
Growing stronger together

TIB DEVELOPMENT BANK
Your Partner for Growth

Amana Bank
Together, on the right path

ILO

unicef

International Organization for Migration (IOM)
The UN Migration Agency

FEED THE FUTURE
The U.S. Government's Global Hunger & Food Security Initiative

UNITED STATES AGENCY INTERNATIONAL DEVELOPMENT
USAID

UNDP

ZANZIBAR SOCIAL SECURITY FUND
ZSSF
Key to the Future

ZBS
ZANZIBAR
BUREAU OF STANDARDS

SHIRIKA LA BIMA
ZANZIBAR INSURANCE CORPORATION

BPRA
ZANZIBAR
BUSINESS AND PROPERTY REGISTRATION AGENCY

ZANZIBAR PRIVATE EMPLOYMENT AGENTS ASSOCIATION
ZANPEA

ZNCC
Zanzibar National Chamber of Commerce

ZANEMA
ZANZIBAR EMPLOYERS' ASSOCIATION

ZANZIBAR TRADE UNION CONGRESS
SOLIDARITY FOREVER
ZATUC

ZRA
ZANZIBAR REVENUE AUTHORITY

# SERIKALI YA MAPINDUZI YA ZANZIBAR



## AFISI YA RAIS, KAZI, UCHUMI NA UWEKEZAJI

**Limetolewa na Kitengo cha Habari na Uhusiano Afisi ya Rais, Kazi, Uchumi na Uwekezaji Zanzibar**

*Mtaa wa Kificho-M/kwerekwe S.L.P 884 Zanzibar*

*Simu namba: 0242230061 Fax: 0242230062*

*Tovuti: www.arkuusmz.go.tz*

*Email : info@arkuusmz.go.tz*

uwekezaji_zanzibar

uwekezajismz.go.tz